# Jarida Maalum

## SHIRIKA LA POSTA TANZANIA

www.posta.co.tz Toleo la 0003 | Aprili - Juni 2022 | Tanzania



# TIMU YA WAHARIRI

**MWENYEKITI**
Macrice D. Mbodo
Postamasta Mkuu, Shirika la Posta
Tanzania

**MRATIBU NA MHARIRI WA JARIDA**
Elia P.K. Madulesi
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano,
Shirika la Posta Tanzania

**MSANIFU WA JARIDA**
Loema Joseph

**WAHARIRI**
Mashala Lufunga Jane Sallu, Rachel
Kitinya &
Khadija M. Suedi

# SALAMU ZA PONGEZI KWA BWANA MACRICE MBODO KWA KUTEULIWA KUWA POSTA MASTA MKUU WA SHIRIKA LA POSTA TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

*Simu: 255-262961500/1*
*Nukushi: 255-262961502*
*Baruapepe : press@ikulu.go.tz*
*Tovuti : www.ikulu.go.tz*

*OFISI YA RAIS,*
*IKULU,*
*1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,*
*CHAMWINO,*
*S.L.P 1102,*
*40400 DODOMA.*

*25 Mei, 2022*
*Accra*

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa Viongozi kama ifuatavyo:-

a) Amemteua Bi. Sauda Kassim Msemo kuwa Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania. Kabla ya uteuzi huu, Bi. Sauda alikuwa Kamishna wa Fedha za Nje, Wizara ya Fedha na Mipango. Bi. Sauda anachukua nafasi ya Dkt. Bernard Yohana Kibesse ambaye ameteuliwa kuwa Balozi.

Uteuzi huu unaanza tarehe 01 Juni, 2022.

b) Amemteua Mhandisi Cyprian John Luhemeja kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO). Mhandisi Luhemeja ni Mtendaji Mkuu, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA).

c) Amemteua Bwana Macrice Daniel Mbodo kuwa Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania *(TPC)*. Kabla ya uteuzi huo, Bwana Mbodo alikuwa Kaimu Postamasta Mkuu, Shirika la Posta Tanzania (TPC).

Uteuzi huu unaanza mara moja.

ZuhuraYunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu.






# NAPE: WEKENI MKAZO KWENYE HUDUMA KUKIDHI HAJA YA WANANCHI

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mh. Nape Nnauye, amelitaka Shirka la Posta Tanzania (TPC) kuendelea kuboresha utendaji kazi wake ili kuhakikisha linakidhi na kutoa huduma stahiki kulingana na mahitaji ya wananchi.

Akizungumza katika halfa ya utiaji saini wa makubaliano ya ushirikiano wa kibiashara kati ya TPC na Shirika la Posta Oman, Nape amesema: "Watendaji wa TPC wekeni mkazo katika utoaji wa huduma kukidhi mahitaji ya sasa ya wananchi. Huduma hizo zisiwe na shaka bali ziwe zenye ubora."

Hafla hiyo ilifanyika Mei 31, 2022 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

Waziri Nape amesema ushirikiano kati ya TPC na wenzao wa Oman utaleta manufaa kwa taifa kwa kuwa wananchi wakipata mwamko wa kutumia huduma za posta, ndivyo Serikali itakavyoongeza mapato kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaunga mkono juhudi zinazoendelea kufanywa na TPC katika kukuza uhusiano na mataifa mengine duniani; akatumia fursa hiyo kuwapongeza wahusika wa posta za Tanzania na Oman kwa kuona fursa katika ushirikiano kati ya mataifa haya mawili, akisisitiza kupanua wigo kila wanapoona fursa.

Niwahakikishie kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mh. Samia Suluhu Hassan inaunga mkono juhudi hizi za pamoja mnazozifanya na iko tayari kushirikiana ninyi kuhakikisha maono mliyonayo yanatimia kwa faida ya nchi hizi mbili," amesema Mh. Nape.

Katika hatua nyingine, Waziri Nape ametumia fursa hiyo kuwakaribisha wageni kutoa Oman kutembelea vivutio vyautalii vilivyopo nchini, ikiwemo Zanzibar pamoja na mbuga mbalimbali za wanyama wakajionee fahari ya Tanzania, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Rais katika kutangaza utalii.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Jim Yonazi, amesema moja ya mikakati inayofanywa na Serikali ni kuhakikisha uwekezaji unaofanywa na TPC unaleta ushindani ndani ya nchi na ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, huku Shirika la Posta likiwa kitovu cha biashara ukanda huu.

Postamasta Mkuu wa TPC, Macrice Mbodo, amesema ushirikiano huu wa kibiashara unalenga kuboresha huduma za 'Duka Mtandao', uchapishwaji wa stampu za pamoja sambamba na kubadilishana ujuzi wa kiteknolojia za utoaji wa huduma za posta kwa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Posta ya Oman, Bw. Nasser Al Sharji, amesema kuungana kibiashara kati ya mashiriki ya nchi hizi mbili, kutarahisisha utumaji wa fedha kwa njia ya usafirishaji wa anga, hususan kwa raia wa nchi hizi. "Vilevile Tanzania itapata fursa ya kuunganishwa na masoko makubwa duniani ikiwemo yale ya Alibaba na Amazon," amesema Bw. Al Sharji.













# DK. KHALID MOHAMED, UJUMBE WA OMAN WAKUTANA

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Mh. Dk. Khalid Salum Mohamed amekutana na ujumbe wa Shirika la Posta Oman ukiongozwa na Postamasta Mkuu, Bw. Nasser Al Sharji.

Ujumbe huo ulifika Zanzibar Juni Mosi mwaka huu kwa ziara ya kitali visiwani, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan, katika kutangaza vivutio vilivyopo nchini.

Katika mkutano huo, Dk. MOhamed ameelezea kufurahishwa kwake na mageuzi yanayoendelea kufanywa na TPC na kupongeza juhudi zilizopo katika kuboresha huduma zake na kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Kwa upande wake, Postamasta Mkuu, Macrice Mbodo, amesema: "Shirika la Posta Tanzania sambamba na Posta ya Oman tumejipanga kushirikiana na SMZ katika kutangaza vivutio vya utalii kwa kutumia stempu tunazozitengeneza; lengo likiwa ni kukuza sekta ya utalii katika mataifa yote mawili."

Bw. Mbodo amemema stempu hizo zitakuwa na vivutio kadhaa, kama majengo ya kihistoria yaliyopo Zanzibar, zikiwa na nafasi ya kupata fursa ya kuuzwa na kupatikana kilakona ya dunia kupitia wakusanyaji wa stempu zaidi ya 60 waliopo Zanzibar, hivyo kukuza na kuitangaza sekta ya utalii nchini.

Mtendaji Mkuu wa Shirika la Posta Oman, Bw. Al Sharji, amesema Shirika la Posta Oman liko tayari kushirikiana na Tanzania kuwafikishia wananchi huduma za posta zilizo bora na zinazoendana na mahitaji yao.

Ikumbukwe kuwa ziara hii ni matokeo ya makubaliano ya kibiashara yaliyofanyika siku moja nyuma, yaani Mei 31, 2022 kati ya taasisi hizi mbili yenye lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma katika mataifa ya Tanzania na Oman.



# RAIS SAMIA ATEMBELEA POSTA YA OMAN

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan, ametembelea Shirika la Posta Oman kujionea utendaji wa shiriki hilo.

Tukio hilo lilifanyika Juni 14, 2022 wakati wa ziara ya kikazi ya Mama Samia nchini humo, siku chache baada ya kusainiwa kwa mkataba wa Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) wa kibiashara baina ya Shirika la Posta Tanzania (TPC) na Shirika la Posta Oman katika maeneo mbalimbali ya kibiashara ili kuleta ufanisi na kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Itakumbukwa kuwa Mei 31, 2022 jijini Dar es Salaam, Tanzania, TPC na Shirika la Posta Oman walitiliana saini makubaliano ya ushirikiano wa kibiashara kwenye maeneo 17 ikiwemo 'Biashara Mtandao', huduma za usafirishaji pamoja na uchapaji stempu za kihistoria; ikizingatiwa kuwa nchi hizi zina uhusiano wa miaka mingi.







# "MIJADALA IJIKITE KWENYE JITIHADA ZA KUBORESHA UZALISHAJI"

Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania (TPC), Macrice Mbodo, amewataka wajumbe wa Baraza la Majadiliano la TPC kutumia majadiliano hayo katika kujadiliana, kukubaliana na kushauri kwa pamoja namna sahihi ya kuboresha utendaji, hususan uzalishaji wa mapato, faida na uchangiaji wa shirika kwenye uchumi na maendeleo ya taifa.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa Baraza la 33 la Majadiliano la Shirika katika ukumbi wa Hoteli ya Naivara jijini Tanga Mei 5, 2022, Bw. Mbodo amesema: "Mijadala ijikite zaidi kwenye kuboresha utendaji wa shirika kwani utendaji unapoimarika hufungua fursa ya kujadili maslahi ya wafanyakazi, maana haki siku zote huendana na wajibu."

Aidha, Kaimu Postamasta Mkuu ametumia kikao hicho kueleza kwa kina dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuifanya posta kuwa ya kidijitali kwa biashara endelevu kupitia mpango mkakati mpya wa nane wa kibiashara unaotarajiwa kuanza kutekelezwa rasmi Julai, 2022.

Katika hatua nyingine, Bw. Mbodo amewashukuru wafanyakazi wote wa TPC nchini na viongozi wote wa vyama vya wafanyakazi kwa mchango mkubwa wanaoendelea kuutoa katika mageuzi ya Shirika yanayoendelea kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa namna bora ndani na nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Baraza la Majadiliano la TPC, Bw. Omari M. Dibibi, amempongeza Kaimu Postamasta Mkuu kwa utendaji wake na kumshukuru kwa kukubali kufungua kikao hicho na kumuahidi kukiendesha kwa weledi na tija ili kuleta matokea chanya kwa Shirika na taifa kwa ujumla kama ilivyokusudiwa.



Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Baraza, Mabruki Makame, amewataka wafanyakazi wote wa Shirika kufuata misingi ya kazi na kuunga mkono maono yaliyomo kwenye mpango mkakati mpya wa Shirika kama ilivyofafanuliwa na Kaimu Postamasta Mkuu.

Naye Msemaji Mkuu wa Wafanyakazi, Junus Ndaro, amepongeza juhudi zinazoendelelea kufanywa na Shirika pamoja na mikakati mizuri iliyopo ya kuboresha utendaji na kuwasihi wajumbe na wafanyakazi wote kuunga mkono kikamilifu utekelezaji wa mikakati hiyo.



# TPC YASHIRIKI UZINDUZI WA RELI YA SGR TABORA

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa ameweka jiwe la msingi la ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha Makutupora - Tabora kitakachogharimu Sh trilioni 4.6 kinachotarajiwa kujengwa kwa miezi 42 ikiwemo minne ya majaribio.

Tukio hilo lilifanywa na Profesa Mbarawa Aprili 12, 2022 mkoani Tabora kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan.

TPC ikiongozwa na Kaimu Meneja Mkuu Uendeshaji Biashara, Constantine Kasese, ikiwa ni wadau wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), imeshiriki hafla hiyo kudhihirisha ukweli kwamba miundombinu boro ya reli hurahisisha kufikisha huduma za Posta mahali popote zinapohitajika.

Shirika limetumia nafasi hiyo kutangaza na kutoa huduma kwa wananchi mbalimbali walioshiriki hafla hiyo kupitia banda lake la maonesho mjini Tabora.

Kabla ya uwekaji rasmi wa jiwe la msingi la ujenzi wa SGR kipande cha Makutupora - Tabora, Profesa Mbarawa amekagua mabanda mbalimbali likiwemo la TPC ambako alipata maelezo ya huduma zinazotolewa na Shirika nchini.



"Nendeni **mkatumie ujuzi** na **utaalamu** mtakaoupata hapa kwa juhudi na maarifa katika kuhakikisha **Shirika linakuwa imara** na kutoa **huduma katika ubora** unaostahili," Mabongo



# BRIGEDIA MABONGO: KATUMIENI UJUZI MLIOPATA KUTOA HUDUMA BORA

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Posta Tanzania (TPC), Brigedia Jenerali (mstaafu) Yohana Mabongo, amewataka viongozi wa TPC kutumia ujuzi watakaopata katika mafunzo ya utekelezaji wa usimamizi wa ubora wa ISO 9001:2015 kuhakikisha Shirika linatoa huduma bora zenye tija kwa taifa.

Brigedia Mabongo ameyasema hayo alipokuwa akifungua mafunzo kwa Menejimenti ya Shirika mkoani Morogoro, Aprili 4, 2022.

"Nendeni mkatumie ujuzi na utaalamu mtakaoupata hapa kwa juhudi na maarifa katika kuhakikisha Shirika linakuwa imara na kutoa huduma katika ubora unaostahili," amesema.

Brigedia Jenederali (mstaafu) Mabongo ameitaka Menejimenti ya Shirika kuhakikisha kila kinachofanyika katika utoaji wa huduma za Posta kuwe chenye ubora unaostahili na chenye tija kulingana na mahitaji ya wadau wote.

Amesisitiza mafunzo hayo yawe chachu ya kuhakikisha usalama na kasi ya utoaji huduma kwa wananchi, hususani usalama wa mizigo, barua na vifurushi vya wateja vinafika kwa wakati ikizingatiwa kuwa uwepo wa Mfumo wa Anwani za Makazi utarahisisha ufikishwaji wa huduma hadi mahali mteja alipo.

"Muongozo huu wa viwango vya ubora wa ISO 9001:2015 una lengo la kuhakikisha usalama katika kutoa huduma, hivyo kwa upande wa huduma, Shirika lihakikishe linalinda na kufikisha mizigo, barua na vifurushi vya wateja kwa usalama mpaka mahali husika kwa kutumia Mfumo wa Anwani za Makazi unaotekelezwa kwa sasa," amesisitiza Brigedia Jenerali.

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ameipongeza Menejimenti kwa kutambua umuhimu wa Shirika kuanza kutumia utaratibu wa viwango vya ubora vinavyolitambulisha Shirika kimataifa, akisema kwa kufanya hivyo TPC itaweza kutoa huduma zenye ubora zaidi kwa wananchi.

Ameahidi kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Menejimenti ya TPC katika kuhakikisha Shirika linatoa huduma bora na zenye viwango vya kimataifa kutimiza mpango mkakati wake ili kuongeza mapato na kukidhi vigezo vya ubora kwa wateja wake.

Kwa upande wake, Kaimu Postamasta Mkuu wa TPC, Macrice Mbodo, amemshukuru Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi kwa kufika kwake na kufungua mafunzo hayo, akisema mafunzo yatakayotolewa kwa viongozi yataongeza tija katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Bw. Mbodo amemuahidi Brigedia Jenerali Mabongo kuwa yeye na Menejimenti watahakikisha wanayatumia vyema mafunzo hayo kukidhi mahitaji ya wadau wote.

"Na ikiwa ni mara yako ya kwanza kuzungumza na Menejimenti hii, nami nikuahidi kuwa tutahakikisha, kupitia mafunzo haya, Shirika linaongeza ufanisi katika kuongeza ubora wa huduma zake," amesema Mbodo.

Mkuu wa Kitengo cha Ubora wa Huduma za TPC, David Andrea, ameushukuru uongozi kwa kukubali na kuona umuhimu wa kuendesha mafunzo anayoamini kuwa yataliwezesha Shirika kuongeza masoko na kurahisisha biashara baina yake na mataifa mengine.

Mafunzo ya viwango vya ubora wa ISO 9001:2015 yalianza mwanzoni mwa Machi 2021 chini ya usisimamizi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Ni moja ya vipaumbele vya kutekeleza mpango mkakati wa saba wa biashara ulioanza mwaka 2019/2020 hadi 2021/2022 ambapo Shirika la Posta Tanzania limeweka malengo ya kuhakikisha linaingia kwenye orodha ya taasisi zinazotoa huduma kwa viwango vya ubora wa kimataifa duniani.

# TANZANIA YAONGOZA KIKAO CHA UPU BERN, SWITZERLAND




Tanzania imeshiriki Mkutano wa Baraza la Uendeshaji la Umoja wa Posta Duniani (UPU) uliofanyika jijini Bern, Uswisi, Mei 9 hadi 13 mwaka huu.

Katika Mkutano huo, Tanzania imeongoza kikao cha Kamati Namba 2 inayohusika na masuala ya Huduma za Posta na Biashara Mtandao (Physical Services and E-commerce) ya Baraza la Uendeshaji la Umoja (Postal Operation Council - POC) kwa kushirikiana na Uswisi wakati wa mikutano ya Baraza la Uendeshaji la umoja huo.

Mwenyekiti wa kikao hicho cha Kamati Namba 2 cha POC alikuwa Bw. Constantine Kasese, ambaye ni Kaimu Meneja Mkuu Uendeshaji Biashara wa Shirika la Posta Tanzania (TPC), akishirikiana na Mwenyekiti mwenza, Bw. Aime Theubet wa Posta ya Uswisi.

Ujumbe wa Tanzania umewakilishwa na maofisa kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na Shirika la Posta Tanzania

Tanzania ni mjumbe wa POC na Baraza la Utawala la UPU ambapo kwa mara ya kwanza katika historia, Tanzania ilifanikiwa kuchaguliwa kuingia kwenye mabaraza yote mawili muhimu ya uamuzi katika Mkutano Mkuu uliofanyika jijini Abidjan, Ivory Coast, Agosti mwaka jana.



# UJUMBE WA TANZANIA WAKUTANA NA MKURUGENZI MKUU WA UPU BERN, SWITZERLAND

Ujumbe wa Tanzania uliohudhuria kikao cha Baraza la Utawala (CA) la Umoja wa Posta Duniani (UPU) kilichofanyika Mei 16, 2022 Makao Makuu ya UPU, Bern nchini Uswisi, umekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa UPU, Bw. Masahiko Metoki.

Ujumbe huo uliongozwa na Bw. Mohammed Khamis Abdulla, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, aliyeambatana na Dk. Jabir Bakari, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) pamoja na wataalamu kutoka wizarani, TCRA, na Shirika la Posta Tanzania (TPC).

Katika mazungumzo hayo, Naibu Katibu Mkuu Bw. Abdulla amempongeza Bw. Metoki kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa UPU wakati wa Mkutano Mkuu uliofanyika Agosti mwaka jana nchini Ivory Coast.

Pia amemshukuru kwa kuwa nchi yake (Japan) iliiunga mkono Tanzania hadi kuchaguliwa kwenye mabaraza muhimu ya uongozi; Baraza la Utawala na la Uendeshaji ya UPU, nafasi zilizoiwezesha Tanzania kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati Namba 2i ya Baraza la Uendeshaji la UPU.

"Sambamba na hilo, ninakushukuru pia kwa kuwa Februari mwaka huu, Tanzania tulipokea Dola za Marekani 208,000 kwa ajili ya kuboresha huduma za posta kupitia mfuko wa Ubora wa Huduma (UPU Quality of Service Fund), amesema Bw. Abdulla.

Naibu Katibu Mkuu ameishukuru UPU kwa kuendelea kuiamini Tanzania na kuipa nafasi ya kuwa kituo cha kutegemeza teknolojia kwa nchi za Afrika zinazoongea Kiingereza pamoja na Msumbiji.
Kituo hicho kipo Makao Makuu ya Shirika la Posta Tanzania, jijini Dar es Salaam.

Kwa upande wake, Dk. Jabir Bakari, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, amemweleza Bw. Metoki kuwa Tanzania imepiga hatua katika eneo la Anwani za Makazi, ambapo Mh. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ametoa msukumo maalumu kuhakikisha kila mwananchi anakuwa na Anwani ya Makazi.

"Kwa hiyo ninakuomba uunge mkono juhudi zinazoendelea kwa kusaidia programu zitakazosaidia kurahisisha na kuboresha utekelezaji na matumizi ya Anwani za Makazi nchini Tanania," amesema D. Bakari.

Sambamba na hilo ameomba pia kuungwa mkono katika kujengea uwezo watumishi wa Posta kwa kuwa Shirika la Posta lipo kwenye mageuzi makubwa ya kidijitali. Pia aliomba UPU kuharakisha ukamilishaji wa vifaa vya kupimia ubora wa huduma ambavyo mamlaka ilikuwa imeagiza kutoka UPU.

Kwa upande wake, Bwana Metoki ameahidi kuendelea kufanya kazi na Tanzania kwenye maeneo ya ubunifu kuhusiana na Anwani za Makazi na Postikodi, huduma za Posta za kidijitali na uboreshaji huduma za Posta nchini.

Vilevile amekubali kuongeza nguvu kwenye kituo cha kutegemeza teknolojia kinachohudumia nchi zinazozungumza Kiingereza pamoja na Msumbiji kinachoongozwa na mtaalamu wa TPC kilichopo jijini Dar es salaam.






# TPC, KENYA KUKUZA USHIRIKIANO WA KIBIASHARA MIPAKANI

Shirika la Posta Tanzania (TPC) limeshiriki kikao cha pamoja na Shirika la Posta Kenya (PCK) chenye lengo la kukuza Ushirikano wa kibiashara katika mipaka ya nchi hizi mbili (Cross Border Trade). Kikao hicho kimefanyika Aprili 16 mwaka huu katika mpaka wa Kenya na Tanzania unaojulikana kama Sirari/Isebania.

TPC iliwakilishwa na Jasson C. Kalile ambaye ni Meneja Biashara ya Barua na Usafirishaji, Dongwe J. Dongwe; Meneja wa TPC Mkoa wa Mwanza na Joyce Chirangi; Meneja wa TPC Mkoa wa Mara, huku PCK ikiwakilishwa na Peter Wanyeki; Meneja Huduma za Usafirishaji; Frida Inchoga, Mshauri wa Postamasta Mkuu PCK; James Aboge Mshauri Mwelekezi na Dina Kadondi; Meneja wa PCK Mkoa wa Nyanza. Katika kikao hicho, Mamlaka ya Mapato Kenya (KRA) iliwakilishwa na Anthony Mugo; Meneja KRA Isebania; mpakani kwa upande wa Kenya.




# POSTA YASHIRIKI MAADHIMISHO YA SIKU YA UHURU WA VYOMBO VYA HABARI DUNIANI

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mh. Nape Nnauye, akiambatana na Katibu Mkuu Wizara hiyo, Dk. Jim Yonaz, wametembelea Banda la Shirika la Posta Tanzania (TPC) lililopo katika ukumbi wa Hoteli ya Gran Melia Jijini Arusha wakati wa ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani.

Kilele cha maadhimisho hayo yaliypfanyika jijini Arusha kilikuwa Mei 3, 2022, yakiwa na kaulimbiu; ***"Uandishi wa Habari na Changamoto za Kidijiti".*** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan, ndiye aliyekuwa mgeni rasmi siku ya kilele huku ufunguzi ukifanywa na Waziri Nape.

TPC ilishiriki maadhimisho haya kama mdau wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano nchini, ambapo Shirika lilipata fursa ya kutoa huduma mbalimbali kupitia banda lililokuwa katika viwanja vya Gran Melia jijini Arusha.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya pamoja na wakuu wa taasisi mbalimbali wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Duniani, Mei 3, 2022, katika ukumbi wa mikutano wa Hoteli ya Gran Melia, jijini Arusha. Kwa mara ya kwana maadhimisho haya yaliwaleta nchini wadau wa habari kutoka mataifa yote ya Afrika. Wa tano Kulia ni Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Macrice Mbodo.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan, akipata maelezo ya huduma zinazotolewa na Shirika la Posta Tanzania kutoka kwa Kaimu Meneja Mkuu Uendeshaji Biashara wa Shirika, Bw. Constantine Kasese (kushoto), alipotembelea Banda la Posta wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani katika Ukumbi wa Mikutano wa Hoteli ya Gran Melia, jijini Arusha. Wa pili kulia ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mh. Nape Nnauye.

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, akitembelea Banda la Shirika la Posta Tanzania na kupata maelezo ya huduma zinazotolewa na Shirika kutoka kwa Kaimu Meneja Mkuu Uendeshaji Biashara, Constantine Kasese, wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Duniani, Mei 3, 2022 katika ukumbi wa mikutano wa Hoteli ya Gran Melia, jijini Arusha.





# TPC, TUTUME WASAINI MAKUBALIANO YA KIBIASHARA

Shirika la Posta Tanzania (TPC) na Kampuni ya Usafirishaji (TUTUME) wamesaini mkataba wa makubaliano ya kushirikiana kibiashara unaolenga kurahisisha na kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya nchini. Hafla hiyo ilifanyika Juni 29, 2022 jijini Dar es Salaam na kushuhudiwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Me. Nape Nnauye.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mh. Nape amezitaka taasisi hizi mbili kuwajibika kwa weledi na kuwa waaminifu katika nafasi zao ili wananchi wapate huduma stahiki kulingana na mahitaji yao. "Muwe na weledi, uaminifu na upendo. Hivi vipewe kipaumbele katika nafasi zenu ili Watanzania wafaidike kwa kupata huduma bora na kwa wakati kila mahali ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," amesema Mh. Nape.

Makubaliano hayo yatawezesha kupanua wigo wa huduma za kijamii, hususan katika sekta ya afya, ambapo TPC kupitia uzoefu wake katika nyanja za usafirishaji, itashirikiana na TUTUME kusafirisha bidhaa kama dawa na sampuli za damu za binadamu na wanyama, pamoja na sampuli za mimea kwa ajili ya vipimo kwenye maabara na hospitalini, hivyo kuwezeha kufanyika kwa urahisi utafiti wa dawa na chanjo.

Waziri amelipongeza Shirika kwa jitihada linazozifanya kwa kushirikisha wadau wa sekta mbalimbali, ikiwepo sekta binafsi, lengo likiwa ni kupeleka huduma karibu zaidi na jamii.

Akizungumza katika hafla hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Jim Yonazi, amesema zipo fursa mbalimbali ambazo TPC Shirika la Posta inaweza kuzitumia kuwafikia wananchi wengi, hususan katika sekta za usafirishaji na utalii; ambapo kupitia utengenezwaji wa stempu, kuna nafasiya kuhamasisha utalii ndani na nje ya nchi.



# MAOFISA HABARI WA SERIKALI WAKUTANA TANGA

Shirika la Posta Tanzania kama mdau wa mawasiliano nchini limeshiriki katika kikao kazi cha moafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano wa Serikali kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Hoteli ya Regal Naivera, jijini Tanga.

Kikao hicho cha siku tano kilifunguliwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mh. Nape Nnauye, Mei 9, 2022. Lengo la kikao hiki ni kuwajengea uwezo maofisa hao, namna ya kutangaza shughuli za Serikali na kuhakikisha Idara/Vitengo vya Mawasiliano na Uhusiano Serikalini vinaimarishwa kuendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Sita na teknolojia mpya ya mawasiliano katika kuwahudumia wananchi.

Aidha, wakiwa Tanga, maofisa habari wametembelea mradi wa maendeleo ya Serikali wa ujenzi wa Bandari ya Tanga unaolenga kukuza bandari iiwezeshe Tanzania kupokea meli kubwa zaidi hivyo kukuza uchumi nchini. Shirika la Posta limewakilishwa na Maofisa Habari wake ambao ni Rachel Kitinya, Loema Joseph na Khadija Suedi



# ANWANI ZA MAKAZI KURAHISISHA HUDUMA ZA POSTA TANGA

Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Jim Yonazi, akizungumza wakati wa ziara yake ya ukaguzi wa upatikanaji huduma za Mawasiliano na Utekelezaji wa Operesheni Anwani za Makazi, Mei 12, 2022, katika makazi mapya ya Kijiji cha Msomera, kilichopo Kata ya Misima, Handeni mkoani Tanga.

Dk. Yonazi amewataka wananchi kuhakikisha wanaweka Anwani za Makazi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma pale watakapohitaji. Ameongeza kuwa, mfumo huo utawawezesha wananchi kufikishiwa mizigo, vifurushi pamoja na huduma nyingine za posta kwa urahisi na uhakika zaidi.





# MBODO AFUNGUA MAFUNZO YA MANUNUZI, UGAVI

Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania (TPC), Bw. Macrice Mbodo, amefungua mafunzo ya Sheria ya Ununuzi wa Umma na uandaaji wa Mpango wa Manunuzi wa Shirika kwa mwaka 2022/2023, Makao Makuu ya Shirika jijini Dar es Salaam.

Mafunzo hayo yaliyofanyika Aprili 8, 2022 yalilenga kuwajengea uwezo watumishi wa TPC katika maeneo hayo, lakini pia ni sehemu ya utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na marekebisho yake ya mwaka 2016 pamoja na Kanuni za Manunuzi wa Umma za mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016.

Pia ni utekelzaji wa miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wataalam wa Kada ya Manunuzi (PSPTB). Aidha, Bw. Mbodo amewataka washiriki wa mafunzo kuzingatia watakayojifunza na kujiandaa kwa utekelezaji wa vitendo ili kuleta tija ndani ya Shirika na kwa maslahi mapana ya taifa.

Mafunzo hayo yameratibiwa na uongozi wa TPC huku wawezeshaji wakiwa ni wataalamu kutoka PSPTB ambao ni Amos Kazinza na Jackson Musiba.



# BALOZI ATEMBELEA MAKAO MAKUU YA SHIRIKA LA POSTA TANZANIA (TPC)

Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani, Dk. Abdallah S. Possi, ametembelea Shirika la Posta Tanzania (TPC) na kufanya mazungumzo na Kaimu Postamasta Mkuu, Bw. Macrice Mbodo.

Ziara hiyo imefanyika Aprili 14, 2022 Makao Makuu ya Shirika, Dar es Salaam, ambapo pamoja na mambo mengine, Dk. Possi alipata nafasi ya kushirikisha uzoefu wake kwenye utendaji wa Posta kutoka mataifa mengine, ikiwemo Ujerumani. Dk. Possi amefurahishwa sana na mageuzi makubwa ya kidijitali yanayofanywa na Shirika la Posta Tanzania.

Kwa upande wake, Bw. Mbodo amemshukuru Balozi Possi kwa kuwa mzalendo na kutumia muda wake kuja makao makuu kujionea mageuzi ambayo Posta imeyafanya.

Bw. Mbodo amemweleza Balozi Possi historia ya Posta; shirika lilikotoka, lilipo na linakokwenda.




# POSTA KINARA MAONESHO YA MOROGORO

*Yakabidhiwa tuzo kwa kushika nafasi ya kwanza kundi la taasisi za Serikali.*

Shirika la Posta Tanzania (TPC) limeshiriki kwenye Maonesho ya Tano ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi yaliyofanyika Mei 9 hadi 14, 2022 kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Maonesho haya yalionesha shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mifuko na Programu mbalimbali za kuwezesha wananchi kiuchumi na pia kuelimisha wananchi namna mifuko hiyo inavyowezesha wananchi na wajasiliamali kiuchumi kwa lengo la kuwajengea uwezo kwa kuwapatia mikopo na dhamana za mitaji na kufunguliwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mh. Martin Shigela, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Biashara na Viwanda Dk. Ashatu Kijaji.

Katika maonyesho haya, Shirika la Posta Tanzania limeibuka kidedea kwa kushika nafasi ya kwanza kwenye kundi la taasisi za Serikali na kutunukiwa ngao na cheti maalumuu cha ushindi. Ushindi huo umechagizwa na utoaji wa huduma kwa njia za kidijitali zilizoboreshwa na zinazoendana na mabadiliko ya kiteknolojia, ikiwemo huduma za Duka la Mtandaoni na Sanduku la Posta la kidijitali (Virtual Box).

Huduma hizi za kidijitali ndizo zilizovuta hisia na hamasa kwa wananchi waliotembelea Banda la Posta na kusababisha wajiunge na huduma hizo za kisasa. Maonesho hayo yalifungwa na Waziri wa Uwekezaji, Biashara na Viwanda Mh. Dk. Ashatu Kijaji kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan.



# SHIRIKA LA POSTA YATIKISA WIKI YA WAMACHINGA DODOMA

Shirika la Posta Tanzania limeshiriki mafunzo kwa Viongozi wa Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA) yanayotolewa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Center (JKCC), jijini Dodoma.

Mafunzo hayo yaliyoongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Bi. Zainab Chaula, yalilenga kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo na machinga katika matumizi ya kidijiti, mifumo ya kiteknolojia, faida za Anwani za Makazi na Biashara Mtandao. Yamefanyika Mei 16 hadi 20 mwaka huu.

Aidha, Shirika la Posta Posta limeshiriki mafunzo hayo kama mmoja wa Wadhamini Wakuu na Mtoa mada wa mafunzo hayo , ambapo kupitia Meneja Masoko wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Amos Milinga na Meneja Biashara Mtandao wa Shirika la Posta Bw. Kulwa Fifi walitoa wasilisho la Shirika hilo na namna litakavyoshirikiana na Wamachinga katika kuendesha Biashara mtandao.

www.posta.co.tz

Let's Go!




Tanzania Posts Corporation
Head Office: Posta House 12th Floor, 7 Ghana Street
P.O.Box 9551, 11300 Dar es Salaam, tanzania
Fax: (022) 2113081 | Phone: 2113394/ 2111715/ 2118280
Mobile: +255 738 070 702 | Email: pmg@posta.co.tz
Web: www.posta.co.tz


@posta_tz